



**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MKOA WA GEITA**



HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE

(Unapojibu tafadhali taja).

Kumb.Na.E.40/7/41

13/10/2021

YAH: TANGAZO LA KAZI.

Kwa mujibu wa kibali cha ajira mpya chenye Kumb.Na. FA. 170/521/01`B`/70 ya tarehe 13 Septemba, 2021 kilichotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe anawatangazia wataanzania wote wenye sifa za kuomba nafasi ya kazi kama ifuatavyo:-

1. Katibu Mahsusii III TGS B1 (Nafasi 01)

Sifa ya Mwombaji.

- Awe amefaulu elimu ya Kidato cha nne.
- Awe amehudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu.
- Awe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja.
- Awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika programu **Windows, Microsoft Office, Internet, E- mail na Publisher.**

2. Kazi na majukumu ya Katibu Mahsusii III TGS B1 :-

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- Kusaidia kutunza kumbukumbu, taarifa za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba za kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi anamofanyia kazi na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, Nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo Ofisi.
- Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa waliopo katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.


3. Masharti ya waombaji wote.

1. Kila mwombaji ahakikishe anaambatanisha vivuli vya vyeti vyake halisi vya Kidato cha Nne, Vyuo na cheti cha kuzaliwa.
2. Kila mwombaji aambatanishe nakala ya taarifa binafsi (CV).
3. Kila mwombaji aambatanishe picha za rangi (passport size 2 zenye jina la mwombaji nyuma).
4. Awe raia wa Tanzania.
5. Awe hajawahi kupatikana na makosa ya jinai na kuhukumiwa.
6. Asiwe na umri wa miaka zaidi ya 45
7. Asiwe amewahi kuachishwa kazi kwa makosa ya nidhamu na Kugushi Vyeti.
8. Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, Hati ya matokeo ya kidato cha nne **HAVITAKUBALIWA.**
9. Waombaji watakao kidhi vigezo ndiyo watakaoitwa kwenye usaili.
10. Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoainishwa hayatashughulikiwa.
11. Ikumbukwe kuwa kuwasilisha vyeti vya uongo vya Elimu na ujuzi (Forgery Certificates) ni kosa la jinai kwa mujibu wa Sheria za Nchi.

12. **Mwisho wa kutuma maombi ni Tarehe 16/11/2021 saa 9:30 Jioni.**
13. Maombi yote yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza na kuwasilishwa Ofisi ya Masjala Bayana iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe au kutumwa kupitia Posta kwa Anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe,
S.L.P 02,
BUKOMBE.

Imetolewa na:-



Lutengano G. Mwalwiba
Mkurugenzi Mtendaji (W)
BUKOMBE

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUKOMBE

Nakala: Katibu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira Katika
Utumishi wa Umma,
S.L.P 2320,
DODOMA

Katibu Tawala (M)
S.L.P 315
GEITA

Mbao za matangazo za Halmashauri zote Mkoa wa Geita.

Mbao za matangazo ofisi za kata zote.